## UIMARISHAJI WA MIFUMO YA SEKTA ZA UMMA (PS3)

USAID
KUTOKA KWA WATU WA MAREKANI

# MRADI WA UIMARISHAJI WA MIFUMO YA SEKTA ZA UMMA (PS3)
# KUIMARISHA UTENDAJI WA KAMATI ZA SERIKALI ZA MITAA NA USHIRIKISHWAJI WA WANANCHI
# MPANGO KAZI WA WAHESHIMIWA MADIWANI KWA MWAKA 2016/17

| Eneo la kuimarisha | Changamoto Zilizoibuliwa | Lengo/Matarajio | Hatua za utekelezaji/Afua | Watu/washirika watakaohusika | Chanzo cha taarifa (Uhakiki) |
|---|---|---|---|---|---|
| **1. Kuimarisha utendaji[1] wa kamati** | | | | | |
| **Baraza la Madiwani** | Wakati mwingine vikao havifanyiki kwa mujibu wa ratiba, kanuni za kudumu za halmashauri na sheria. | Vikao vya Baraza la Madiwani kufanyika kwa mujibu wa sheria, kanuni za kudumu za utumishi na ratiba. | Kushauriana na Mkurugenzi kupanga bajeti ya kutosha kwa ajili ya vikao vya Baraza kwa mujibu wa kanuni za kudumu za Halmashauri na ratiba . | Mwenyekiti na Mkurugenzi wa Halmashauri, Karani wa kamati na afisa rasilimali watu. | Karani wa kamati wa Halmashauri, Washauri Daftari la mihtasari |
| | Wajumbe kutokupewa nyaraka husika siku saba kabla ya kikao | Madiwani kupewa nyaraka husika kama ilivyoamriwa kisheria (Kwa wakati) | • Kushauriana na Mkurugenzi wa Halmashauri kuandaa mapema nyaraka za Baraza.<br>• Karani wa kamati kusambaza mwaliko na nyaraka zote mhimu kwa wakati. | Diwani, Mwenyekiti wa Halmashauri, karani wa kamati na afisa rasilimali watu. | Karani wa Kamati, Washauri?/Daftari la mihtasari |
| | Wananchi kutotaarifiwa mapema kuhusu vikao vya Baraza ili waweze kuhudhuria kwa wingi | Taarifa kuhusu vikao vya Baraza la Madiwani zitolewe kwa umma kwa muda uliopangwa kama inavyobainishwa katika sheria ya serikali za mitaa. | • Ratiba ya vikao vya Baraza ibandikwe kwenye maeneo ya wazi ngazi za kata, vijiji/mitaa na kwnenye tovuti.<br>• Kuhamasisha wananchi wahudhurie Baraza<br>• Kurejesha na Kuimarisha rejista ya wananci kwa ajili ya vikao vya baraza. | Diwani, wenyeviti wa vijiji na mitaa, maafisa watendaji wa kata na vijiji na mitaa. | • Washauri/Nakala ya matangzo ya vikao vya baraza.<br>• Rejista ya jamii kurejeshwa na kutumika katika mamlaka zote za serikali za mitaa |

[1] Kumbuka: Utendaji ina maana kuboresha usimamizi pamoja na kufuata kanuni na sheria za kamati, na ushirikishwaji wa wananchi ikiwa ni pamoja na kuingiza michango ya wananchi katika mipango na maamuzi

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | Wananchi kutokupewa fursa ya kutoa mchango wao kwa maandishi wakati wa vikao vya baraza ingawa wana haki ya kufanya hivyo. | Wananchi wanapewa fursa ya kuchangia kwa mandishi maswali na kero zao kwa mujibu wa sheria. | Kuanzisha rejista kwa ajili ya kurekodi maswali na kero za wananchi wakati wa kikao cha Baraza la Madiwani. | Diwani, Mwenyekiti , Mkurugenzi , wa Halmashauri, wenyeviti wa vijiji, na karani wa kamati | • Nakala za matangzo ya vikao vya baraza..<br>• Rejista ya jamii<br>• Rejista ya maswali na hoja za wananchi |
| | Vikao vya Baraza kufanyika makao mkuu y Halmashauri kila mara na kutotoa fursa kwa wananchi waishio maeneo mbalimbali huhudhuria vikao vya baraza kutokana na umbali. | Halmashari huandaa utaratibu wa kufanya vikao vya Baraza katika maeneo mbambali ndani ya wilaya endapo huduma zinazokidhi . | Kubaini maeneo na taasisi zenye miundombinu inayoweza kuruhusu kikao cha Baraza la Madiwani kufanyika. Mfano kumbi za shule makanisa n.k | Mwenyekiti na Mkurugenzi wa Halmashauri Mtunza hazina na Karani wa kamati na wadau wengine wa maendelo | Washauri kujadili uwezekano wa kutekeleza<br>Daftari la mihtasari ya baraza |
| **Kamati za kudumu Ngazi ya Halmashauri** | • Vikao vya Kamati za kudumu havifanyiki kulingana na ratiba, kanuni za kudumu za utumishi na sheria.<br>• Wadau wakuu, mf. sekta binafsi, AZAKI na wadau wa mendeleo (DPs) hawaalikwi kwenye kamati ya kudumu | • Mikutano ya kamati za kudumu ifanyike kulingana na sheria na kanuni<br>• Wadau wakuu wanaalikwa pale wanapohitajika. | • Wenyeviti wa Kamati za kudumu kufuatilia kuhakikisha kuwa ratiba za kamati zinazingatiwa.<br>• Kufuatilia na kuhamasisha wadau wakuu wahudhurie vikao vya kamati mbalimbali pale wanapopta mialiko. | Diwani, Mkurugenzi wa Halmashauri, Wenyekiti wa kamati za kudumu, karani wa kamati, mtunza hazina na mkuu wa idara ya rasilimali watu | Washauri, Daftari la mihtsari ya vikao vya kamatimihtasari |
| **Kamati ya Maendeleo ya Kata (KMK) au WDC** | • Vikao havifanyiki kulingana na sheria na ratiba.<br>• Mahudhurio hafifu<br>• Ukosefu wa kanuni za kudumu au sheria ndogo za kuongoza uendeshaji wa KMK<br>• Mara nyingi ajenda za KMK haziibuliwi kutoka ngazi za vijiji/mitaa au vituo vya huduma na/au mrejesho kutoka kwenye halmashauri. | • Vikao vinafanyika kwa mujibu wa sharia, kanuni na ratiba.<br>• Kuwepo Kanuni za kudumu au sheria ndogo za kuongoza uendeshaji wa kamati ya kata<br>• Ajenda za kamati ya maendeleo ya Kata ziibuliwe kutoka kwenye vijiji au mitaa na vituo vya huduma. | • Diwani kuhamasisha Maafisa Watendaji wa Kata waandae vikao.<br>• Kuhamasisha wenyeviti wa vijiji wahudhurie.<br>• Mrejesho kutoka kwenye baraza kuhusu taarifa za Kamati ya Maendeleo ya Kata upatikane kwa wakati.<br>• Kuhamasisha watendaji wa kata, vijiji na mitaa na wakuu wa vituo vya huduma waibue ajenda kutoka maeneo yao vijiji, mitaa na vituo vya huduma. | • Diwani<br>• Mkuu wa idara ya rasilimali watu<br>• Karani wa kamati wa Halmashauri<br>• Afisa watendaji wa Kata, Viijiji Mitaa<br>• Afisa Tarafa<br>• Walezi wa Kata<br>• Wakuui wa vituo vya huduma | Washauri/ Mtu mahsusi kwenye PS3, faili la mihtasari za vikao. |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| **Ngazi ya Kijiji/ Mtaa**<br>**1. Mkutano Mkuu wa Kijiji** | • Mikutano haifanyiki kama inavyotakiwa kisheria na miongozo<br>• Wananchi wengi hawahudhuriib mikutano hii<br>• Hakuna mwogozo, kanuni au sheria ndogo kuongoza mikutano hii | • Mikutano inafanyika kwa mujibu wa sharia, kanuni na miongozo.<br>• Wananchi wanahamasika kuhudhuria mkutano<br>• Upo mwongozo wa namna ya kuendesha mkutano mkuu wa kijiji. | • Diwani kuhamasisha wenyeviti wa vijiji na Maafisa watendaji wa vijiji kuandaa ratiba za vikao.<br>• Mikutano itoe taaarifa zitakazowahamasisha wannanchi kuhudhuria<br>• Kuandaa mwongozi au kanuni za uendeshaji wa mikutano husika Kuhamasisha jamii wahudhurie vikao. | • Diwani<br>• Maafisa watendaji wa vijiji / mitaa<br>• Wenyeviti wa vijiji | , mtu mahsusi kwenye PS3, mshauri, faili la mihtasari mihtasariya mikutano ya vijiji/mitaa |
| **2. Mabaraza ya vijiji** | • Vikao havifanyiki kwa mujibu wa kisheria<br>• Hakuna ratiba ya mabaraza au haizingatiwi<br>• Hakuna kanuni au mowngozo wa kuendesha mabaraza ya vijiji | • Vikao vinafanyika kwa mujibu wa sheria na miongozo.<br>• Ratiba ipo na inafuatwa<br>• Uwepo wa kanuni au mwongozo wa mabaraza ya vijiji. | • Diwani kuhamasisha wenyeviti wa vijiji na maafisa watendaji wa vijiji waandae ratiba za vikao<br>• Kuandaa na kutekeleza sharia ndogo ndogo za ukusanyaji wa mapato<br>• Kuandaa kanuni ama mwongozo wa kuongoza mabaraza ya vijiji. Na mitaa | • Diwani<br>• Mkurugenzi wa halmashuri<br>• Mwanasheria<br>• Maafisa watendaji wa vijiji/Maafisa watendaji wa mitaa na wenyeviti wa vijiji. | Washauri, mtu mahsusi kwenyePS3 na faili la mihtasari ya mabaraza ya vijiji |
| **3. Kamati za vijiji** | • Vikao havifanyiki kama inavyotakiwa kisheria<br>• Hakuna ratiba ya vikao vya kamati au haizingatiwi<br>• Hakuna kanuni au mwongozo wa kuendesha kamati hiizo. | • Vikao vya kamati za vijiji vinafanyike kisharia<br>• Kuwepo kwa ratiba inayofuatwa.<br>• Kuwepo kwa kanuni au mwongozo wa uendeshaji wa kamati | • Madiwaani kuhamasisha watendaji wa kata na vijiji waandae ratiba ya kamati<br>• Kuandaa na kutekeleza sharia ndogo ndogo za za vijiji za ukusanyaji mapato | • Maafisa watendaji wa vijiji/maafisa watendaji wa mitaa na wenyeviti wa vijiji. | Washauri, mtu mahsusi kwenyePS3 na faili la mihtasari za vikao vya kamati za vijiji/mitaa |
| **Mikutano ya hadhara ya madiwani** | • Mahudhurio ya wananchi kwenye vikao hayatoshi.<br>• Itikadi za kisiasa zinaathiri mahudhurio.<br>• Ukosefu wa mfumo rasmi wa madiwani wa kukutana na wapiga kura wake. | • Mikutano ya hadhara ya madiwani ifanyike kama inavyotakiwa.<br>• Diwani awe na ratiba na mihtasari za mikutano ya hadhara | • Madiwani wanaanda mikutano ya hadhara katika kila kijiji/mtaa<br>• Watendaji wa kata wanaandaa ratiba za ratiba za mikutano ya hadhara kwa waheshimiwa madiwani na kusambaza vijini/mitaaa | • Diwani<br>• Maafisa watendaji wa kata na vijiji<br>• Wenyeviti wa vijiji | Washauri, mtu mahsusi kwenye PS3 na faili la mihtasari za vikao.<br>Ratiba za madiwani za mikutano ya hadhara |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| **Kamati/Bodi za vituo vya huduma**[2] | • Baadhi ya kamati za uangalizi hazijaundwa Vikao havifanyiki kulingana na sheria na miongozo<br>• Miongozo haigusii masuala muhimu ili kuziwezesha zitende kazi kwa ufanisi.<br>• Hakuna uhusiano wa moja kwa moja kati ya kamati za vituo vya kutolea huduma na kamati za vijiji. | • Kamati/Bodi za vituo vya huduma zinaundwa vizuri<br>• Bodi/kamati za vituo zifanye kazi kwa ufanisi zaidi.<br>• Uhusiano wa moja kwa moja kati ya kamati za vituo vya kutolea huduma na kamati za kijiji. | • Watendaji wa Kata, vijiji na mtaa waandae ratiba za vikao na kusambaza kwa wananchi<br>• Kurekebisha na kusambaza miongozo kuhusu uundwaji kamati na utendaji wake.<br>• Kushawishi uwepo wa mahusiano kati za kamati vya huduma na kamat za vijiji | • Diwani<br>• Mkurugenzi wa halmashauri<br>• Afisa mtendaji wa kijiji<br>• Wenyeviti wa vijiji<br>• Wakuu wa vituo vya huduma | Washauri, mtu mahsusi kwenyePS3 na faili la mihtasari za vikao vya bodi au kamati za vituo vya kutolea huduma |
| **2. Utoaji wa taarifa kwa wananchi kuongeza uwazi na uwajibikaji**[3] | | | | | |
| **Uwazi/utoaji taarifa na uwajibikaji** | • Hitaji la kutoa taarifa kwa umma halijatekelezwa kikamilifu<br>• Ukosefu wa miongozo ya utoaji taarifa<br>• Ukosefu wa utamaduni wa kujisomea miongoni mwa wanajamii.<br>• Wananchi hawajahamasishwa kudai taarifa.<br>• Taarifa zitolewazo ni za kitaalam sana kiasi kwamba wananchi hawawezi kuzielewa.<br>• Matumizi hafifu ya teknolojia ya kisasa ya mawasiliano , tovuti radio za jamii (community radio). Magazeti, majarida n.k | • Utekelezaji wa hali ya juu wa hitaji la kutoa taarifa kwa umma.<br>• Miongozo ya utoaji taarifa iwepo.<br>• Ongezeo la madai ya taarifa kutoka kwa wananchi.<br>• Taarifa rafiki kwa watumiaji zipatikane kwa wananchi kwa wakati na kwa njia muafaka.<br>• Kuhimiza matumizi ya TEHAMA na kuboresh utaratibu wa kuaanda na kuweka taarifa kwenye tovuti za halmashauri | • Mweyekiti na mkurugenzi kusimamia ili wenyeviti wa vijiji na maafisa watendaji wa vijiji kufanya vikao kwa mujibu wa ratiba.<br>• Kuandaa miongozo ya utoaji taarifa.<br>• Kuhamasisha wananchi wadai na kuzitumia taarifa.<br>• Kujengea uwezo wa namna ya kuandaa taarifa rafiki na zenye kuwavutia watumiaji<br>• Kuhamsiha jamii kudai na kutumiai taarifa za kielectroniki kupitia simu zao za mkononi, na tovuti. | • Diwani<br>• Mkurugenzi wa halmashauri<br>• Afisa mtendaji wa kijiji<br>• Wenyeviti wa vijiji<br>• Msimamizi mkuu wa kituo<br>• Maafisa wa TEHAMA | Washauri, Mtu mahsusi kwenye PS3, tovuti, mbao za matangazo, radio za jamii n.k. |
| **3. Kuboresha mifumo ya utoaji mirejesho kuongeza ushiriki wa wananchi kupitia njia za utoaji malalamiko, masanduku ya maoni na mikutano ya hadhara** | | | | | |

[2] Kamati za shule (P) , Bodi za shule (S),kamati za vijiji za watumiaji wa maji, Kamati za wafugaji, kamati za ardhi, baraza la ardhi la kijiji, kamati za zahanati, Bodi za vituo vya afya/hospitali, Kamati ya maafa.

[3] Kumbuka: utoaji wa taarifa unaelezwa kuwa unahusisha njia nne—kupitia kamati au watoa huduma (k.m. mbao za taarifa, mikutano ya hadhara, vipeperushu); intaneti (k.m. mitandao, majukwaa ya hadhara ya serikali za mitaa); vyombo vya habari vya ndani (k.m. machapisho, redio, runinga); na njia za jadi (k.m ngoma na maigizo)

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| **Ushughulikiaji wa matatizo na maoni ya wananchi** | • Masanduki ya maoni kutokufanya kazi kutokana na kukosekana au kutozingatiwa mwongozo wa sanduku la maoni.<br>• Mfumo rasmi wa kushughulikia malalamiko haupo (dawati la malalamiko, rejesta ya malalamiko, timu, n.k)<br>• Jamii hazijaelimishwa kuhusu uwepo na taratibu za matumizi ya madawati ya malalamiko | • Kufufua matumizi ya sanduku la maoni na taratibu zake<br>• Kuanzisha na kuimarisha mfumo wa kushughulikia malalamiko/maoni ya wananchi katika ngazi zote za halmashauri<br>• Kutoa elimu kwa jamii kuhusu uwepo na taratibu za matumizi ya madawati ya malalamiko . | • Kusambaza miongozo juu ya masanduku ya maoni kwa Halmashauri hitaji<br>• Kusambaza mwongozo wa kushughulikia malalamiko kwa Halmashauri zote<br>• Kutoa mafunzo kuhusu taratibu za kuanzisha na kuendesha dawati la malalamiko<br>• Kuhamasisha jamii juu ya matumizi ya mfumo wa kutoa malalamiko | • Diwani<br>• Mkurugenzi wa halmashauri<br>• Afisa tarafa<br>• Afisa mtendaji wa kata, Afisa mtendaji wa mtaa/Afisa mtendaji wa kijiji. | Mtu mahsusi kwenye PS3 na mshauri kumfuatilia diwani ili kupata taarifa juu ya masanduku. |
| **4. Kuimarisha ushirikishwaji wa wananchi katika kuandaa mipango kwa kutumia njia ya fursa na vikwazo vya maendeleo** | | | | | |
| **Ushiriki wa wananchi katika kuandaa mipango** | • Ushirikishwaji mdogo wa wananchi katika kuandaa mipango yao ya maendeleo<br>• Ufahamu mdogo juu ya mchakato wa fursa na vikwazo vya maendeleo miongoni mwa wafanyakazi wa Halmashauri na wananchi kwa ujumla<br>• Timu za kuwezesha utekelezaji wa mfumo wa fursa na vikwazo vya maendeleo katika ngazi ya kata na kijiji/mtaa hazipo au hazifanyi kazi.<br>• Miradi iliyoibuliwa katika mchakato wa fursa na vikwazo na kupewa kipaumbele na wananchi kutojumuishwa katika mpango wa maendeleo na bajeti ya halmashauri.<br>• Kukosekana kwa mrejesho juu ya vipaumbele vya miradi ya wananchi. | • Wananchi wanashiriki katika kuandaa mipango yao ya maendeleo<br>• Elimu itolewe kwa watendaji na raia juu ya mfumo wa fursa na vikwazo vya maendeleo katika ngazi ya kata, kijiji na au mtaa<br>• Timu za uwezeshaji mfumo wa fursa na vikwazo vya maendeleo katika ngazi ya kata na kijiji/mtaa kufufuliwa na kuimarishwa<br>• Miradi ya vipaumbele vya jamii inajumuishwa kwenye mpango wa maendeleo wa H/W.<br>• Wananchi wapewe mrejesho kuhusu vipaumbele walivyobainishs. | • Kujenga uwezo wa kutekeleza mfumo wa fursa na vikwazo vya maendeleo katika ngazi za kata na kijiji.<br>• Kuhuisha timu za kuwezesha utekelezaji wa mfumo wa fursa na vikwazo vya maendeleo katika ngazi za kata, kijiji/mtaa.<br>• Kuhamasisha wanajamii washiriki katika kutekeleza mfumo wa fursa na vikwazo vya maendeleo na shughuli zingine za maendeleo.<br>• Kutenga fedha zaidi za kugharamia miradi ya jamii zitokazo kwenye vyanzo vya serikali za mitaa na serikali kuu.<br>• kutoa mrejesho kwa wananchi kuhusu matokeo ya mipango iliyopita. | • Diwani<br>• Mkurugenze wa Halmashauri<br>• Afisa Tarafa<br>• Afisa Mtendaji Kata, Afisa Mtendaji wa Mtaa/Afisa Mtendaji wa kijiji. | Mtu mahsusi kwenye PS3 na mshauri kumfuatilia diwani ili kupata taarifa za utekelezaji wa mfumo wa fursa na vikwazo vya maendeleo. |